KUZUNGUMZA MBINU ZA DHARURA – **Maswali ya kujadili:**

MASWALI
YA KIKUNDI

# Mbinu za 'KUZUIA'

Ukiukwaji wa dharura ni ukiukaji wa haki unaowaathiri watu maalum, katika maeneo maalum, na kwa wakati maalum. Mifano ni kama hotuba za chuki, unyanyasaji mitaani, uharibifu wa sehemu za ibada, unyanyasaji wa polisi, au kukamatwa kiholela.

– Je, tunashuhudia ukatili wa 'dharura' katika jamii yetu (katika maeneo ya umma, binafsi, au mtandaoni)?

– Je, matukio haya hutokea katika maeneo na nyakati zinazotabirika, kama vile mtandaoni, mitaani, kwenye sehemu za ibada, vituo vya polisi, au wakati wa sherehe za kidini?

– Bungua bongo hatua ambazo zingetumika kuzuia ukiukwaji wa 'dharula' katika jamii yetu. Je, kuna vitu tunaweza kufanya kama binafsi, kwa kushirikiana katika vikundi au mashirika? Autunaweza kuwahamasisha wengine kama vile mamlaka za mitaa au polisi kuchukua hatua? Andika mawazo yako ya hatua kwenye vikaratasi vya gundi (wazo moja kwa kila karatasi moja na kubandika).

KIPINDI CHA 6 KITINI

KUZUNGUMZA MBINU ZA DHARURA – **Maswali ya kujadili:**

MASWALI
YA KIKUNDI

# Mbinu za 'KUSIMAMA NA KUOKOA'

Ukiukwaji wa dharura ni ukiukaji wa haki unaowaathiri watu maalum, katika maeneo maalum, na kwa wakati maalum. Mifano ni kama hotuba za chuki, unyanyasaji mitaani, uharibifu wa sehemu za ibada, unyanyasaji wa polisi, au kukamatwa kiholela.

– Je, tunashuhudia ukatili wa 'dharura' katika jamii yetu (katika maeneo ya umma, binafsi, au mtandaoni)?

– Tunaweza kuingilia kati na kukomesha aina yoyote ya ukatili sisi wenyewe, au kuokoa watu? Muda gani ni salama kuingilia kati na kwa namna gani?

– Kipindi gani hatupaswi kuingilia zaidi ya kuomba msaada na kuonya watu?

– Bungua bongo hatua ambazo zingetumika kusimamisha ukiukwaji wa 'dharula' katika jamii yetu. Je, kuna vitu tunaweza kufanya kama binafsi, kwa kushirikiana katika vikundi au mashirika? Autunaweza kuwahamasisha wengine kama vile mamlaka za mitaa au polisi kuchukua hatua? Andika mawazo yako ya hatua kwenye vikaratasi vya gundi (wazo moja kwa kila karatasi moja na kubandika).

MASWALI YA KIKUNDI

KUZUNGUMZA MBINU ZA DHARURA – **Maswali ya kujadili:**

# Mbinu za 'OMBA MSAADA/ONYA'

Ukiukwaji wa dharura ni uvunjaji wa haki unaowaathiri watu maalum, katika maeneo maalum, na kwa wakati maalum. Mifano ni kama hotuba za chuki, unyanyasaji mitaani, uharibifu wa sehemu za ibada, unyanyasaji wa polisi, au kukamatwa kiholela.

- Je, tunashuhudia ukatili wa 'dharura' katika jamii yetu (katika maeneo ya umma, binafsi, au mtandaoni)?
- Katika hali gani tunaweza kuhitaji kuomba msaada kwa ajili yetu wenyewe au wengine, au kuwaonya watu kuhusu hatari? Msaada kutoka kwa nani unaweza kuwa wa manufaa, na ni nani tunayepaswa kuwaonya? Je, tunajua jinsi ya kuwasiliana nao? Tuna uhusiano nao wa kutosha ili iwe rahisi kuwapata?
- Bungua bongo hatua ambazo zingechukuliwa kuhakikisha kwamba msaada unapatikana kwa ajili ya na watu walioonywa wakati dharula imetokea. Je, kuna vitu tunaweza kufanya kama binafsi, kwa kushirikiana katika vikundi au mashirika? Autunaweza kuwahamasisha wengine kama vile mamlaka za mitaa au polisi kuchukua hatua? Andika mawazo yako ya hatua kwenye vikaratasi vya gundi (wazo moja kwa kila karatasi moja na kubandika).